

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA (MKATABA) KWA KADA YA UDEREVA NAFASI SABA (7)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wale wenye sifa ya udereva nafasi saba (7). Kazi hii itakuwa ni ya mkataba wa miezi mitatu na mshahara utalipwa kwa mujibu wa Kisahihisho “C” cha Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 20 wa Mwaka 2002 Nyongeza VI.

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI:-

Dereva Daraja la II – Nafasi saba (7), Ngazi ya Mshahara TGS B ambayo ni sawa na Sh. 390,000.00 kwa mwezi.

- Mwombaji awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV)
- Mwombaji awe na Leseni ya Daraja la E/C₁ ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Mwombaji awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Mwombaji mwenye Cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II atafikiriwa kwanza.

KAZI ZA KUFANYA

- Kukagua gari kabla na baada ya kuanza safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa zote katika daftari la safari (Log Book)
- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

2.0 MASHARTI YA JUMLA:-

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi 45.
- Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya Taaluma, Kidato cha Nne, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) za “Passport Size” za hivi karibuni na iandikwe majina yote ya mwombaji kwa nyuma.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **28 Februari, 2020**

3.0 MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
Ukumbi wa Jiji,
S.L.P. 9084,
1 – Barabara ya Morogoro,
11882 – DAR ES SALAAM.



Sipora J.Liana
MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM